

Mpango wa Kurudi Shuleni¹ unatoa matarajio na viwango vya Idara ya Elimu na Makuzi ya Awali ya Watoto kwa ajili ya utendaji usalama wa shule za umma katika kipindi cha ugonjwa ulioenea wa COVID-19. Madhumuni ya mpango huu ni kupunguza uwezekano wa kuenena kwa COVID-19 huku pia ikitoa elimu bora na huduma za wanafunzi.

Idara, wilaya za shule na shule zitafanya kazi kwa ushirikiano ili kuwasaidia wanafunzi na walimu. Mwendelezo wa mkazo utawekwa katika kuhakikisha mawasiliano thabiti na ya wazi, kutoa fursa kwa ajili ya ujifunzaji wa kiweledi na kuhimiza uvumbuzi darasani.

MAHUDHURIO YA SHULE NA UKUBWA WA KUNDI

1. Chekechea mpaka Gredi 2

- Muda wote shuleni pamoja na mwalimu;
- Punguzo la ukubwa wa kundi, karibia 15 kila inapowezekana; na
- Watoto walio ndani ya makundi wanaweza kuingiliana lakini wanapaswa kujitenga na makundi mengine.

2. Gredi la 3 mpaka 5

- Muda wote shuleni pamoja na mwalimu;
- Punguzo la ukubwa wa kundi, kila inapowezekana; na
- Watoto walio ndani ya makundi wanaweza kuingiliana lakini wanapaswa kujitenga na makundi mengine.

3. Gredi la 6 mpaka 8

- Muda wote shuleni pamoja na mwalimu;
- Ukubwa wa darasa la kawaida; na
- Watoto walio ndani ya makundi wanaweza kuingiliana lakini wanapaswa kujitenga na makundi mengine.

4. Gredi la 9 mpaka 12

- Hudhuria shuleni kwa utaratibu wa zamu (angalau kila baada ya siku);
- Punguzo la idadi ya wanafunzi kwa darasa ili kuzingatia kujitenga kimwili; na
- Kujitenga kimwili kwa wanafunzi na wafanyakazi wa shule kwa mita moja ndani ya darasa. Wanafunzi hawatawekwa makundini kutokana na ratiba na chaguo za kozi.

Wakati ambapo wanafunzi wa Gredi la 9 mpaka 12 hawapo kimwili shuleni, watahusishwa katika mbinu mchanganyiko za ujifunzaji, kwa kutumia njia mbalimbali za ufundishaji ikiwemo ujifunzaji wa mtandaoni, miradi yenye mwongozo na ujifunzaji wa kiuzoefu.



Kujitenga kimwili

Ingawa [kujitenga kimwili kwa mita moja](#) kutahitajika katika darasa la Gredi la 9 mpaka 12, umbali wa mita mbili utahimizwa katika maeneo ya pamoja katika ngazi zote za gredi. Hii inahusika wka wafanyakazi wa shule na wanafunzi wanapokuwa nje ya madarasa yao.

Wafanyakazi wa shule watahakikisha upangaji ratiba unalenga kupunguza msongamano na kuhakikisha makundi ya wanafunzi yanaheshimiwa kipindi cha mapumziko, chakula cha mchana na utembeaji wao ndani ya shule.

¹ Waraka huu utarekebishwa kadri itakavyohitajika ili kuakisi taarifa mpya kabisa za afya ya umma. Tafadhali rejelea tovuti ya Idara ya Elimu na Makuzi ya Awali ya Watoto kwa ajili ya waraka wa hivi kabibuni kabisa. Malekezo haya yanaweza pia kubadilika kulingana na Hali ya Hatari na Amri ya Utekelezaji wa Lazima.

MIPANGO YA ELIMU KWA MWEZI SEPTEMBER 2020

Madhumuni yaliyopangwa ya ujifunzaji yatakuwa ya lazima kwa mwaka wa shule wa 2020-21. Mtaala maalum unaoweka mkazo kwa wanafunzi kupata matokeo ya msingi utatumika. Kutakuwa na punguzo la mwingiliano darasani kati ya wafanyakazi wa shule na wanafunzi kwa wanafunzi wa Gredi la 9 mpaka 12. Muda unaotumiwa kimwili darasani unaweza kutofautiana kati ya magredi na shule.

Shule na wilaya za shule zitaandaa shule, magredi na madarasa ili kuwasilisha mtaalama kwa kuzingatia makundi na kujitenga kimwili. Maelekezo zaidi ya afya na usalama yatatolewa kwa wilaya ya shule na wafanyakazi wa shule mapema kadri iwezekanavyo.

TAARIFA YA ZIADA:

- Nafasi zote zilizopo ambazo zinawezesha ujifunzaji zitatumiwa ili kuunga mkono ujifunzaji. Wilaya za shule hazikatazwi kutumia nafasi za nje ya shule au za jumuiya ili kuwezesha ujifunzaji.
- Shule zitapangilia upya madarasa yao kwa namna itakayoendeleza kujitenga kimwili ndani ya madarasa.
- Shule zitapangilia upya maeneo yao ya pamoja ili kuhakikisha kujitenga kimwili kati ya makundi ya wanafunzi.
- Shule zinaweza kuangalia suala la kuunganisha madarasa na kutumia makundi ya magredi mchanganyiko.

GREDI LA 9 MPAKA 12

- Wanafunzi watakuwa wakijifunza katika muundo mchanganyiko wa kielimu na kuhudhuria shule kimwili kwa utaratibu wa zamu angalau kila baada ya siku moja. Wasipokuwepo shuleni, wanafunzi wataendelea kujifunza wakiwa mbali.
- Walimu watapewa wanafunzi kuakisi ukubwa wa kawaida wa darasa.
- Walimu watawajibika kwa darasa lao zima, ama wawepo kimwili au wanahusishwa katika shughuli mchanganyiko za ujifunzaji.
- Walimu wanawajibika kuandaa matokeo ya ujifunzaji kwa wanafunzi ili wayafikie wasipokuwepo darasani (k.m., ujifunzaji wa kiuzoefu, kulingana na mradi au wa mtandaoni).
- Walimu watahitajika kuhakikisha wanafunzi wa nyumbani wana nyenzo za ujifunzaji na rasilimali muhimu au wanafundishwa moja kwa moja mtandaoni.
- Kulingana na upatikanaji, wanafunzi wanaweza kuhimizwa kuchukua kozi za mtandaoni, fursa za ujifunzaji wa kiuzoefu na mbinu nyingine za ujifunzaji (ushirikiano na aina nyingine) ili kukidhi matokeo ya ujifunzaji. Chaguo nyumbufu za kozi zinapaswa kupatikana kwa wanafunzi.
- Teknolojia itatumika ili kutegemeza ujifunzaji. Idara inafanya mapitio ya chaguo ili kuwezesha ujifunzaji wa mbali wakati wanafunzi wanapokuwa hawapo kimwili shuleni.
- Shule zinahimizwa kuangalia ratiba zao za kila siku na kila wiki ili kuona kama zinaweza kuboreshwa ili kupunguza mwingiliano kati ya wanafunzi na kuzingatia maelekezo yao ya afya na usalama.

USALAMA WA WAFANYAKAZI NA WANAFUNZI WALIO HATARINI

Wafanyakazi wa shule na wanafunzi ambao ni sehemu ya watu walio hatarini wanahimizwa kushauriana na watoa huduma wao wa afya ili kubaini kama wanaweza kuhudhuria shule. Wanafunzi ambao hawawezi kuhudhuria shule kutokana na tatizo la kiafya wataandaliwa mpango wa ujifunzaji na mwalimu wao mteule kwa ajili ya usaidizi wa kielimu.



Mpango wa Utendaji

Kila shule ya umma, kwa kushauriana na waratibu wa Wilaya ya Shule wa Afya na Usalama Kazini, wataandaa Mpango wa Utendaji wa COVID-19, kabla ya kufunguliwa shule, unaoainisha jinsi shule itakavyosimamia shughuli za kila siku huku ikizingatia viwango vya ziada. Mpango huu wa utendaji, unaoidhinishwa na wilaya ya shule, utaelezea taratibu za namna makundi ya wanafunzi yatakavyofanya shughuli na kutembea shuleni (hasa katika maeneo ya msongamano na maeneo ya pamoja kama vile makabati, maliwatoni, vyumba vya kubadilisha nguo, nk.) na kupanga suala la kuleta/kuchukua wanafunzi. Utajumuisha pia taarifa kuhusu saa za shule za utendaji na kipindi cha mpito cha shule pamoja na utekelezaji wa itifaki za afya na usalama.